ANNUAL NGOs FORUM 2023 DODOMA

RISALA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA TAIFA LA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NACONGO) DKT. LILIAN BADI

Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI);

Mhe. Selemani Jafo (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira;

Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.), Waziri wa Fedha;

Waheshimiwa Mawaziri wengine mliopo hapa;

Mhe. Bi. Mwanaidi Khamis, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;

Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

Dkt. Self Abdallah Shekalaghe, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum;

Ndugu Makatibu Wakuu wengine mliopo hapa;

Bi. Mwantumu Mahiza, Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

Mhe. Fatma Tawfik (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;

Bi. Vickness Mayao, Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

Bw. Ahmed Khalid Abdulla, Mrajis wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali Zanzibar;

Bw. Stephen Okello, Mkurugenzi Mtendaji, Ofisi ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Uganda;

Bw. Revocatus Sono, Katibu Mkuu wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO);

Bw. Hassan Khamis Juma, Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Asasi Zisizo za Kiserikali Zanzibar (ANGOZA);

Ndugu Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali mliopo hapa;

Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;

Mhe. Neema Lugangira, Mbunge anayewakilisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM);

Waheshimiwa Wabunge na Madiwani mliopo hapa;

Mhe. Didier Chassot - Balozi wa Uswisi nchini;

Mhe. Emilio Rossetti - Kaimu Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini;

Mwakilishi wa Ubalozi wa Uingereza;

Mwakilishi wa Ubalozi wa Canada;

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO);

Wawakilishi wa Balozi mbalimbali hapa nchini;

Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la USAID;

Ndugu Wakuu wa Taasisi na Wawakilishi wa Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo;

Ndugu Wajumbe wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

Ndugu Viongozi, Menejimenti na Watumishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;

Ndugu Wasajili Wasaidizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wa Mikoa na Halmashauri;

Ndugu Wajumbe wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO);

Ndugu Viongozi, Wanachama, Wafanyakazi na Wanufaika wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

Ndugu Viongozi wa Dini;

Ndugu Viongozi wa Kimila;

Ndugu Wanahabari;

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...!

Mheshimiwa Makamu wa Rais, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa salama ilikushiriki Mkutano wa Mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Natambuakuwa eengi wetu hapa wamesafiri kutoka katika mikoa mbalimbali iliwaweze kushiriki katika tukio hili ambalo ni muhimu kwa mustakabali wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Taifa kwa ujumla.

Pili, napenda kutumia nafasi hii kwa niaba ya Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ujumla, kukushukuru kwa moyo wa dhati kabisa kwa kukubali mwaliko wetu na kuja kujumuika nasi leo. Nafahamu una majukumu mengi ya kitaifa, lakini umetoa kipaumbele katika shughuli hii.

Tunakushukuru sana **Mheshimiwa Makamu wa Rais**! Mheshimiwa Makamu wa Rais, napenda pia kuwashukuru sana viongozi, Menejimenti na Watumishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, chini ya uongozi madhubuti wa mwanamke mahiri na jasiri hususani katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na kwa watoto, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb), kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Kipekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayoongozwa na Hajjat Mwantumu Mahiza na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayoongozwa na Bi. Vickness Mayao, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uratibu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara, lakini pia katika uratibu wa maandalizi ya Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka wa tatu mfululizo tangu mwaka 2021 hadi sasa.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, napenda pia kutumia fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali waliofanikisha haya yote tunayoyashuhudia leo. Kwa namna ya kipekee, nitambue mchango wa Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania kupitia SDC, WHO, EU, Ubalozi wa Canada, Shirika la LSF, THRDC, Plan, MDH, LHRC, Amani Girls, CBM, Benki ya NMB, Benki ya CRDB, Montessori, Malala Fund, NCA, Femina Hip, BBC Media Action, BRAC Maendeleo, CCBRT, FCS, Good Neighbors Mercy Corps, NIRAS Tanzania, PDF na TRIAS Tanzania. Wadau wengine ni Turkish Maarif, Water for People, World Renew, Zaina Foundation, Care International, Friends of the Plasta House, PELUM Tanzania, Relief Initiatives, Forum CC, Freedom House, Media 4 Development and Advocacy, Baker Tilly, Internews, SHDEPHA+, Action Aid, Youth Rehabilitation, Food for Children, OIKOS, pamoja na wadau wengine wote ambao kutokana na muda nisingeweza kuwataja, lakini tunatambua umuhimu wao na wametambuliwa pia kwenye baadhi ya mabango ya shughuli yetu. Niseme tu najivunia kuona NaCoNGO imeimarika na kuongeza wadau wengi zaidi. Nawashukuru sana!

Aidha, napenda kuwashukuru viongozi, wawakilishi na wanufaika wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, washirika wa maendeleo na wawakilishi wa sekta binafsi mliopo hapa na hasa wale waliosafiri umbali mrefu kutoka katika mikoa mbalimbali nje ya Dodoma, ili waweze kuhudhuria Jukwaa hili la mwaka 2023. Asanteni sana kwa kushiriki!

Mheshimiwa Makamu wa Rais, kama unavyofahamu, Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini imeendelea kukua na kuimarika mwaka hadi mwaka sio tu kwa idadi ya Mashirika yaliyosajiliwa, lakini pia kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali hususan katika afua za afya, mazingira, ulinzi wa jamii, uwezeshaji wananchi, elimu, kilimo, jinsia, maji, utawala bora na haki za binadamu kama ilivyoainishwa katika kitabu hiki cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022.

Hata hivyo, pamoja na mchango huo mkubwa wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo kwa namna moja au nyingine, zimechangia kupunguza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini. Changamoto hizo zimekuwa zikijirudia mara kwa mara, lakini hatunabudi kuzitaja na sisi kama Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali tupo tayari kushirikiana na Serikali katika kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu:

1. Changamoto ya kwanza ni kuhusu upatikanaji wa vibali, hususanimuda mrefu unaotumika kukamilisha mchakato wa kupata vibali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali hapa nchini;

2. Changamoto ya pili inahusu vigezo vya upatikanaji wa misamaha ya kodi (charitable status) kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo baadhi ya Mashirika yamekuwa yakiwasilisha maombi ya kupatiwa misamaha ya kodi bila mafanikio na pasipo kupatiwa mrejesho wasababu za kushindikana kwa maombi husika;

3. Changamoto ya tatu ni uwepo wa mifumo ya kielektroniki ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambayo haisomani, jambo ambalo linawalazimu wadau kuwasilisha taarifa hizo hizo kwa Mamlakatofauti ndani ya Serikali.

4. Vilevile, baadhi ya wadau wamelalamika kuwa mfumo wa mlipa kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) sio rafiki kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

5. Aidha, changamoto nyingine ni baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa kutozingatia utekelezaji wa Kifungu cha 31(c) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, kinachoyataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa yanayajengea uwezo Mashirika ya ndani kutekeleza afua mbalimbali badala ya wao kuwa watekelezaji wa moja kwa moja wa miradi jambo linalonyima Mashirika ya ndani fursa za kukua na kujiendesha.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, kama ambavyo Serikali imefanikiwa kutatua changamoto mbalimbali katika sekta ya afya, elimu, kilimo, mifugo na uvuvi, pamoja na maeneo mengine, ni mtumaini yetu makubwa kuwa changamoto hizo zitafanyiwa kazi ili kujenga mazingira rafiki na wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi kwa ajili ya maslahi mapana ya wananchi wa Tanzania na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wetu, tunaahidi kuendelea kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kwamba tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria nyingine za Nchi.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa kumalizia, nikushukuru tena, kwa kukubali kujumuika nasi leo, tumejiridhisha pasina shaka kuwa Serikali yetu inayatambua Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwani kwa miaka mitatu mfululizo tumepata Viongozi Wakuu wa Nchi kutusikiliza na kuzungumza nasi, hili ni la kujivunia na kuipongeza sana Serikali yetu sikivu. Tunaomba ufahamu kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatambua kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan hasa katika kuwaletea wananchi maendeleo. Tunaomba sana utufikishie salamu zetu kwa Mheshimiwa Rais.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...!

Asanteni sana kwa kunisikiliza...!

Wathamini Wetu

National Council of NGOs (NaCoNGO)
P.O. Box 2838, Dodoma, Tanzania.
CCT church House (3rd floor), Dodoma
Email: info@nacongo.or.tz